

### 3. مَدُّ الصَّلَةِ الْكُبْرَى Maddusw-Swillatil-Kubraa

Maana ya Swillah<sup>1</sup>

Ni madd inayotokea pale ه (haa) ya kiwakilishi cha mwanaume cha mtu wa tatu (*al-ghaaib*) katika umoja (فَرْد) ikabeba *i'raab* inayonasibiana (kasrah au dhwammah) na inapotanguliwa na herufi iliyo na *i'raab*, kisha kufuatiwa na hamzah katika neno la pili yake.

Hukmu yake ni kuvuta harakah nne au tano sawa na hukmu ya مَدُّ الْجَائِزِ الْمُنْفَصِلِ (maddul-jaaizil-munfaswil).

Inapokuwa na dhwammah	Inapokuwa na kasrah
أَفْتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ <sup>3</sup>	وَمَا وَصَّيْنَا بِهِمْ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ <sup>2</sup>
وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى <sup>5</sup>	وَمِنْ آيَاتِهِمْ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ <sup>4</sup>

<sup>1</sup> Rejea mlango wa مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy)

<sup>2</sup> Ash-Shuwraa (42: 13)

<sup>3</sup> Al-Kahf: (18: 50)

<sup>4</sup> Ar-Ruwam (30: 21)

<sup>5</sup> Al-Layl (92: 11)